## UTANGULIZI

Sheria ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya Na. 5 ya Mwaka 2015 ilianzisha Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya ambayo ilianza kazi rasmi mwezi Februari 2017. Majukumu ya Mamlaka ni kufafanua, kuhamasisha, kuratibu na kutekeleza hatua zote zinazolenga katika udhibiti wa matumizi na usambazaji wa dawa za kulevya. Katika kuelezea majukumu yake kisheria, Mamlaka inafanya kazi zifuatazo:-

1. Kuelimisha na kuhamasisha jamii kuhusu udhibiti wa matumizi na biashara ya dawa za kulevya;
2. Kuandaa na kutekeleza Mpango wa Taifa wa Kudhibiti Dawa za Kulevya;
3. Kuchukua hatua stahiki za kupambana na biashara ya dawa za kulevya zikiwemo kukamata, kupekua na kufanya uchunguzi wa masuala yanayohusu dawa za kulevya;
4. Kuratibu na kuwezesha wadau wanaojihusisha na udhibiti wa matumizi na biashara ya dawa za kulevya pamoja na tafiti kuhusu dawa hizo;
5. Kusimamia utekelezaji wa makabidhiano na mikataba ya kimataifa katika udhibiti wa dawa za kulevya na
6. Kuhamasisha na kuhakikisha kuwa jitihada za ushirikiano wa kimataifa katika kudhibiti dawa za kulevya zinaimarishwa.

Katika kuongeza uelewa wa jamii juu ya Sheria ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya Na. 5 ya Mwaka 2015 dondoo chache muhimu kwa jamii kuhusu makatazo na maelekezo zimeainishwa kama ifuatavyo:-

## MAKOSA YA KUJIHUSISHA NA MATUMIZI YA DAWA ZA KULEVYA

1. Matumizi ya dawa za kulevya adhabu yake ni faini isiyopungua shilingi milioni moja (1), au kifungo cha miaka mitatu (3) jela au adhabu zote mbili kwa pamoja. Hatahivyo, Mahakama inaweza kumpatia Mraibu wa dawa za kulevya aliyetiwa hatiani kwa makosa ya matumizi ya dawa hizo fursa ya kupata tiba ya uraibu chini ya masharti maalum badala ya kuhukumiwa kifungo
2. Kukutwa na kiasi kidogo cha dawa za kulevya kwa matumizi binafsi bangi isiyozidi gramu 50 na mirungi isiyozidi kilogramu 2, faini isiyopungua shilingi laki tano, au kifungo cha miaka mitatu au adhabu zote mbili kwa pamoja.
3. Kukutwa na kiasi kidogo cha dawa za kulevya kwa matumizi binafsi heroin, methamphetamine au cocaine (dawa za viwandani) isiyozidi gramu 2 adhabu yake ni faini isiyopungua shilingi milioni moja, au kifungo cha miaka mitano au adhabu zote mbili kwa pamoja
4. Kumwekea mtu dawa za kulevya kwenye kinywaji au chakula pasipo mtumiaji kujua kosa hilo halina dhamana na adhabu yake ni faini isiyopungua shilingi milioni 50, au, kifungo kisichopungua miaka 30 au adhabu zote mbili kwa pamoja.
5. Kukutwa katika eneo ambalo hutumiwa na watumiaji wa dawa za kulevya bila sababu ya msingi adhabu yake ni faini isiyopungua shilingi milioni moja (1), au kifungo cha miaka mitatu (3) jela au adhabu zote mbili kwa pamoja.
6. Kukutwa na vifaa vinavyotumika kutumia dawa za kulevya kama sindano bila sababu ya msingi adhabu yake ni faini isiyopungua shilingi milioni moja (1), au kifungo cha miaka mitatu (3) jela au adhabu zote mbili kwa pamoja.
7. Kutoa dawa tiba zenye asili ya kulevya bila kuidhinishwa au kuwa na cheti cha daktari kosa hilo halina dhamana na adhabu yake ni faini isiyopungua shilingi milioni 50, au, kifungo kisichopungua miaka 30, au adhabu zote mbili kwa pamoja.

## MAKOSA YA KUJIHUSISHA NA UZALISHAJI WA DAWA ZA KULEVYA

1. Kilimo cha mimea inayozalisha dawa za kulevya (mfano bangi na mirungi) adhabu yake ni kifungo kisichopungua miaka 30
2. Kumiliki mtambo wa kuzalishia dawa za kulevya ni kosa ambalo halina dhamana na adhabu yake ni kifungo cha maisha na faini isiyopungua shilingi milioni 200

## MAKOSA YA KUJIHUSISHA NA BIASHARA YA DAWA ZA KULEVYA

### A. Dawa za Mashambani

1. Kufanya biashara, kusafirisha au kukutwa na bangi au mirungi chini ya kilo 20, ni kosa lenye dhamana na adhabu yake ni kifungo kisichopungua miaka 30.
2. Kufanya biashara, kusafirisha au kukutwa na bangi au mirungi kuanzia kilo 20 hadi kilo 100, ni kosa ambalo halina dhamana na adhabu yake ni kifungo kisichopungua miaka 30.
3. Kufanya biashara, kusafirisha au kukutwa na bangi au mirungi kuanzia kilo 100 na zaidi, ni kosa ambalo halina dhamana na adhabu yake ni kifungo cha maisha.

### B. Dawa za Viwandani

1. Kufanya biashara, kusafirisha au kukutwa na heroin, methamphetamine au cocaine isiyozidi gramu 20, ni kosa ambalo lina dhamana na adhabu yake ni kifungo kisichopungua miaka 30
2. Kusafirisha au kukutwa na heroin, methamphetamine au cocaine kuanzia gramu 20 hadi gramu 200, ni kosa ambalo halina dhamana na adhabu yake ni kifungo kisichopungua miaka 30
3. Kusafirisha au kukutwa na heroin, methamphetamine au cocaine zaidi ya gramu 200, ni kosa ambalo halina dhamana na adhabu yake ni kifungo cha maisha

### C. Dawa Tiba zenye Asili ya Kulevya (Mf. Valium, Tramadol, Pethidine)

Kuuza, kusambaza au kupata dawa tiba zenye asili ya kulevya kwa kutumia cheti cha daktari huku ukijua au ukiamini kuwa cheti hicho kimeghushiwa au kimepatikana isivyo halali au kimetolewa zaidi ya miezi sita iliyopita ni kosa ambalo halina dhamana na adhabu yake ni faini isiyopungua shilingi milioni 50, au, kifungo kisichopungua miaka 30 au adhabu zote mbili kwa pamoja.

### D. Kemikali Bashirifu

1. Kusafirisha au kukutwa na kemikali bashirifu chini ya kilo 30 au lita 30 ni kosa ambalo lina dhamana adhabu yake ni kifungo kisichopungua miaka 30.
2. Kusafirisha au kukutwa na kemikali bashirifu kuanzia kilo 30 au lita 30 hadi kilo 100 au lita 100 ni kosa ambalo halina dhamana na adhabu yake ni kifungo kisichopungua miaka 30.
3. Kusafirisha au kukutwa na kemikali bashirifu zaidi ya kilo 100 au lita 100 ni kosa ambalo halina dhamana na adhabu yake ni kifungo cha maisha.

### E. Uuzaji wa Dawa za Kulevya kwa Watoto au kwenye Taasisi za Umma

Kufanya biashara ya dawa za kulevya kwa watu wenye umri chini ya miaka 18, au kwenye taasisi za elimu, vituo vya huduma za jamii au maeneo yanayozunguka taasisi hizo ni kosa ambalo halina dhamana na adhabu yake ni kifungo kisichopungua miaka 30.

### F. Ufadhili wa Biashara ya Dawa za Kulevya

Kufadhili biashara ya dawa za kulevya ni kosa ambalo halina dhamana na adhabu yake ni kifungo cha maisha na faini isiyopungua shilingi bilioni moja.

### G. Ushiriki wa Kampuni kwenye Biashara ya Dawa za Kulevya

Kampuni ikijihusisha na biashara ya dawa za kulevya, Kiongozi wake ataadhibiwa kulingana na aina ya kosa alilotenda na kampuni itafilisiwa au usajili wake utafutwa.

### H. Kutumika kwa Eneo au Chombo cha Usafiri katika Biashara ya Dawa za Kulevya

Matumizi au biashara ya dawa za kulevya kwenye eneo, jengo au chombo cha usafiri, adhabu yake ni Mmiliki au mwenye mamlaka kutozwa faini isiyopungua shilingi milioni tano (5) au kifungo kisichopungua miaka mitatu (3) au adhabu zote mbili kwa pamoja.

## TARATIBU ZA UTEKETEZAJI WA DAWA ZA KULEVYA

- Bangi na mirungi inayokutwa imelimwa mashambani huteketezwa kwa namna mbalimbali ikiwemo kufyekwa, kukatwa au kuchomwa moto kwa mujibu wa sheria.
- Bangi na mirungi inayokamatwa ikiwa maeneo mengine pamoja na heroin, cocaine, mandrax, dawa tiba zenye asili ya kulevya na kemikali bashirifu, huteketezwa kwa amri ya Mahakama.



*Uteketezaji wa dawa za kulevya*

## SHERIA KUHUSU UTAIFISHAJI MALI

Mamlaka inaweza kushikilia mali zinazohusiana na makosa ya dawa za kulevya kwa ajili ya kufanya uchunguzi ambao unaweza kupelekea mali hizo kutaifishwa na Serikali chini ya Sheria ya Mazalia ya Uhalifu ya mwaka 1994 kama ilivyorejewa mwaka 2019.


**Kimetayarishwa na**

Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya
S.L.P 80327, 8 Barabara ya Kivukoni, 11486 Dar es Salaam
Baruapepe: cg@dcea.go.tz | Tovuti: www.dcea.go.tz

@dceatanzania @dceatanzania @dceatanzania
DCEATV Simu ya Bure 119


**MAMLAKA YA KUDHIBITI NA KUPAMBANA NA DAWA ZA KULEVYA**



# SHERIA YA KUDHIBITI NA KUPAMBANA NA DAWA ZA KULEVYA NAMBA 5 YA MWAKA 2015